
# KISWAHILI NA UTANDAWAZI



Mhariri: Leonard Chacha Mwita

SURA YA TANO

# Magazeti kama Kichocheo cha Kuendeleza Fasihi ya Watoto na Vijana: Mfano kutoka *Daily Nation* Na *Taifa Leo*

Pamela M.Y.Ngugi

**Ikisiri**

*Matumizi ya magezeti kama chombo cha kufunzia darasani ni jambo ambalo limepokelewa na wasomi wengi. Magazeti yanaweza kutumika kama njia moja ya kujaliza na kutimiliza masomo mbalimbali ikiwemo fasihi ya watoto. Lengo la makala hii ni kubainisha mchango wa magazeti katika kuendeleza fasihi ya watoto na vijana. Mchango huu utabainika kwa kuchambua vitanzu mbalimbali vinavyojumuishwa katika magazeti haya na namna vinavyochangia katika kuendeleza fasihi ya watoto.*

## Utangulizi

Babalola (2002) anasema kuwa magazeti ni kitabu cha kaida ambacho hutoa taarifa za hivi karibuni kwa wakati uliopo, taarifa ambazo zinahusu habari za kijamii, kitaifa na kimataifa. Vilevile magazeti hutoa tahakiki ya wakati kuhusu hali ya uongozi na uamuzi unaofanywa na viongozi katika nchi. Pia hutoa taarifa za hivi karibuni kuhusu buradani za muziki, maigizo, televisheni, na hata vichekesho au futuhi ili kuwatumbuiza watu. Kutokana na uamilifu wake wa kuarifu, kufunza na kuburudisha, magazeti yamepokelewa kwa wazi miongoni mwa watu wazima na watoto. Magazeti huweza kuwafikia watu wa matabaka mbalimbali na makundi tofauti ya wanajamii kutokana na sababu kuwa kila kikundi cha jamii kinashugulikiwa katika magazeti haya.

Kwa hakika magazeti yanatumika kama nyenzo ya kuendeleza usomaji miongoni mwa wanajamii. Harakati hii hufanyika kupitia

kusoma, kuandika na hata dayalojia inayotokea kati ya wasomaji na wahakiki, ambayo ni msingi wa kuendeleza lugha kwa njia inayofaa na ya ufanisi. Hivyo basi, magazeti yana uwezo wa kuwapa wasomaji motisha ya kusoma hata zaidi au hata yakawa kichocheo cha kusoma aina mbalimbali ya fasihi wanayokutana nayo.

Kutokana na maendeleo ya kiteknolojia, miundo ya elementi mbalimbali katika gazeti huzingatiwa kwa makini. Elementi kama vile mahali pa kuweka hadithi maalumu, ukubwa wa maandishi wa kila sehemu na picha zinazoambatishwa huzingatiwa kwa makini ili kuwavutia wasomaji wa aina na viwango mbalimbali.

Uamilifu mbalimbali unaotolewa na magazeti ndio kivutio cha watu wa makundi mbalimbali kutaka kuyasoma. Ni kutokana na muktadha huu ambapo makala hii inalenga kubainisha nafasi ya magazeti kama kichocheo cha kuendeleza fasihi ya watoto na vijana na haswa katika kusaidia kujenga tabia ya usomaji miongoni mwao.

## Uhusiano kati ya magazeti na fasihi kidhima

Magazeti yanaweza kutumika kama kichocheo cha kupata mawazo ya kuandika kazi ya fasihi; kwa wale wasomaji waliokomaa. Magazeti yanaweza pia kuchangia katika kuimarisha mbinu za usomaji pamoja na mbinu za kifasihi kupitia kusoma mada mbalimbali na za kisasa na ambazo zimeandikwa kwa mitindo mbalimbali.

Kwa wale wasomaji wasiopenda kusoma au kiwango chao cha usomaji ni kidogo, usomaji wa magezeti unaweza kumpa nafasi ya kusoma mambo mbalimbali bila kushutumiwa kwa vyovyote vile. Kwa upande wa lugha, magazeti humpa msomaji nafasi ya kukumbana na mitindo mbalimbali ya lugha kuanzia kwa maoni ya mhariri hadi kwa lugha ya michezo (Guenther na Bushman 1984).

Rosenblatt (1995) anaamini kwamba usomaji ni mapatano ambayo hudhihirika kwa njia mbili kuu. Njia ya kwanza inahusu ujumi ambao hujumuisha kufikiria, kuhisi na kupata tajriba kutokana na kusoma fasihi. Njia ya pili inahusu kile anachokiita '*efferent*' ambayo inarejelea ile hali ya kupata maarifa kupitia usomaji wa fasihi mbalimbali. Kwa njia hizo basi kila msomaji hufanya mapatano yake kwa sababu tofauti. Kwa sababu hii basi watoto na vijana wanahitaji kupewa nafasi ya kusoma magazeti na vitabu kwa lengo la kufikia aina hizi za mapatano wanayoyafanya katika usomaji wao

Kama tulivyotangulia kueleza hapo awali, magazeti hutelekeza majukumu mbalimbali katika jamii. Majukumu haya si tofauti na yale ambayo yameelezwa na wataalamu mbalimbali wa fasihi ya watoto kuwa fasihi huarifu, hufunza, huonya na kuburudisha. Magazeti kama ilivyo fasihi, hutambua na kurekodi matendo mbalimbali ya wanajamii. Vilevile husimulia hadithi na kutoa ujumbe kuhusu maisha ya kila siku ya binadamu (Babalola 2002). Kwa njia hiyo hiyo, wataalamu wa fasihi ya watoto wamebainisha dhima kadha wa kadha za fasihi ya watoto.

Mojawapo wa dhima hizi ni kujiburudisha. Msomaji aliyebobea katika usomaji anaweza kutambua raha anayohisi katika kusafiri na mhusika fulani pamoja na tajriba anazopitia mhusika huyu katika hadithi. Vivyo hivyo katika gazeti, taarifa zinazotolewa kuhusu hali mbalimbali za maisha huweza kutoa taswira fulani ambapo msomaji atatembea na mhusika huyo katika gazeti.

Dhima ya pili ya kusoma ni kutaka kujiondoa katika hali sumbufu ya maisha anayopitia msomaji. Usomaji wa hadithi ya watoto huwapa nafasi ya kujiliwaza na kujichepua pamoja na kuondoka kwa muda kutoka kwa hali sumbufu za maisha. Dhima hii ni muhimu si tu kwa watoto bali hata kwa watu wazima wanaohitaji kujiliwaza na kujichepua kwa muda kutoka kwa hali ngumu za kimaisha. Kwa vile maudhui yanayopatikana magazetini mara nyingi hayapishani na ya vitabu vya fasihi, hivyo basi magazeti yanaweza kuwa kirejelezi ambacho wanafunzi wanaweza kujitambulisha nacho. Taarifa au habari zinazochapishwa katika magezeti zinaweza kutumika kama mada za uandishi wa kifasihi.

Wasomaji-shabiki husoma kwa sababu wanafahamu kuwa vitabu huchachawiza ubunifu wao. Hadithi tunazozisoma hutufanya kufikiria kuhusu mhusika fulani, mazingira, sababu za kuwepo na mageuzi katika ploti, au kiishio cha hadithi ambacho ni tofauti na matarajio yetu. Vivyo hivyo mada mbalimbali zinazopatikana katika maendelezo hutufikirisha na kuchochea ubunifu wa wasomaji kwa viwango mbalimbali. Katika kuzisoma hadithi za magaeztini, tunaweza kuzitumia katika kulinganisha kwa mfano hadithi hizo na muundo wa hadithi fupi kama utanzu wa fasihi.

Dhima nyingine ya fasihi ni kwamba huwasiadia watoto kujielewa na kuwaelewa watu wengine. Mtoto anakua akijua kuwa wapo watu ambao maisha yao ni tofauti na yake lakini ni muhimu kuwaheshimu na kukubali utofauti huu. Utofauti huu hudhihirika pia katika habari

zinazotolewa kwenye magazeti wakati ambapo matukio mbalimbali kutoka katika jamii tofauti yanapowasilishwa.

Magazeti hutoa habari mpya kuhusu kile ambacho kimetendeka hivi karibuni katika maisha ya binadamu. Matukio kama hayo yanaweza kuwa ni ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na hata kidini. Habari hizi huwa zimekusanywa kutokana na hali halisi ya maisha, hasa kutokana na tajriba za watu hawa ambao kwa pamoja wanaunda jamii na vile vile hueleza mahusiano ya watu hawa (Babalola, 2002). Hivyo basi tunaweza kuchunguza migogoro inayotokea katika fasihi na tukailinganisha na ile inayoripotiwa katika magazeti hasa aina mbalimbali ya migogoro kama vile, mtu na mtu mwenyewe binafsi, mtu na mazingira yake, na mtu na mtu au watu wengine katika jamii.

Watoto husoma ili waweze kujitajribisha na kuelewa umbo la lugha. Watoto wanaweza kutambua matumizi mbalimbali ya lugha kupitia wahusika katika hadithi na baadaye mtoto akapata maarifa ya matumizi ya lugha ambayo yatamsaidia kujieleza vilivyo.

Kupitia magazeti, watoto hasa wa viwango vya chini wanaweza kupewa picha kutoka magezetini na wakaandika sentensi fupi kuhusu picha hizo. Wanafunzi wa viwango vya juu wanaweza kupewa nafasi ya kujadili mada mbalimbali katika gazeti. Katika kufanya hivyo, watakuwa wanasaidiwa kuendeleza kipawa chao cha kusema na hata kujieleza.

Ni kupitia kujua mbinu za unadishi ambapo watoto wanaweza kueleza tajriba zao (Aras 2012). Ikiwa wanatakiwa kuandika chochote kile, basi watakuwa pia wanaendeleza mbinu zao za uandishi. Kwa kifupi, tunaona kuwa majukumu ya fasihi yanahusiana moja kwa moja na yale ya magazeti kwa sababu fasihi na magazeti helenga kuwasilisha ujumbe falani. Kwa upande mwingine kazi mbalimbali za kifasihi pamoja na magazeti zinaweza kutumika kama njia ya kujenga na kuendeleza umakinifu, kuhifadhi habari, kutatua matatizo ya kijamii na kutaka kujua chanzo cha habari fulani.

## Usomaji wa magazeti shuleni na nyumbani

Utafiti uliofanywa na Ngugi (2010) kuhusu hali ya fasihi ya watoto nchini Kenya, hasa katika Kiswahili, ulilenga pia kubainisha tabia ya usomaji wa magazeti miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Matokeo ya utafiti huu yalithibitisha kuwa watoto wanapenda kusoma aina mbalimbali ya magazeti. Miongoni mwa magazeti waliyotaja

kuwa wanayasoma ni pamoja na Daily Nation, Sunday Nation, Taifa Jumapili, Taifa leo, Standard, Sunday Standard, Maneno, Sparkle, Sara (kufuatia orodha hiyo).

Gazeti la Nation lilionekana kupendwa na watoto wengi wanaopata magazeti kwa sababu gazeti hili huwahudumia watoto na vijana kwa kuwa linalenga maudhui mbalimbali yanayowavutia watoto na vijana wa viwango tofauti tofauti. Kwa sasa shirika hili la habari lina mradi wa kuwapelekea watoto magazeti shuleni. Mradi huu ni muhumu kwa sababu utawachochea watoto kusoma si magazeti hayo tu, bali na vitabu vya fasihi.

Mvuto wa gazeti la Nation unatokana na kuwepo kwa mada mbalimbali zinazowavutia watoto pamoja na mbinu za uandishi. Kwa mfano, katika gazeti la Jumamosi, kijigazeti cha Shujaaz huambatanishwa kila majuma mawili. Kijigazeti hiki hutolewa bila malipo. Kwa sasa kijigazeti hiki kimechapisha zaidi ya sura 55 tangu kuzinduliwa kwake. Yaliyomo na namna yanavyowasilishwa yamelenga vijana kati ya umri wa miaka 13 kwenda mbele.

Lugha inayotumiwa ni Sheng ambayo ndiyo lugha inayowatambulisha vijana wengi nchini. Huanda pakawa na mjadala kuhusu kipengele hiki lakini hivyo ndivyo hali ilivyo kwamba sheng ni kijilugha ambacho huwatambulisha vijana si tu katika miji mikubwa bali hata sehemu fulani za mashambani. Kijigazeti hiki huwahimiza vijana kufanya kazi na kutia bidii katika shughuli ambazo zitaweza kuinua maisha yao kiuchumi, huwaeleza umuhimu wa kuchagua marafiki wanaoweza kuwajenga, umuhimu wa kuepuka hali ambazo zitasitisha masomo yao kama vile kupata mimba mapema au kujiingiza katika kutumia madawa ya kulevya na kadhalika. Vile vile kijigazeti hiki huwapa viburudisho kupitia kwa mchongoano ambapo vijana wanapewa nafasi ya kuchangia katika utungaji wa michongoano hiyo.

Katika gazeti la *Daily Nation* na *Sunday Nation* hapakosi sehemu iliyotengewa watoto inayojulikana kama Chidren's Corner. Katika sehemu hii kuna hadithi ambazo zimechapishwa katika kitabu na kila siku mtoto anapewa nafasi ya kuisoma hadithi hiyo ambayo hutokea kila siku kwa visehemu. Lengo ni kujenga taharuki ya mtoto na kumtaka aisome hadithi hiyo siku inayofauata. Mbinu hii ni muhimu kwa wale watoto ambao hawawezi kusoma kitabu wakamaliza.

Wanapohitimisha sehemu ya hadithi wanajiona kuwa wamekamilisha kazi kubwa. Wanafunzi kama hawa watakuwa

wanaanza kujenga mazoea ya kusoma maishani mwao. Watoto wachanga katika shule za chekechea huhudumiwa pia kwa kupewa nafasi ya kukamilisha mchoro mmoja kwa kila siku pamoja na kuwataka waujaze mchoro huo kwa rangi mbalimbali.

Pia, kuna sehemu ya kujenga msamiati wao ambapo watoto wanatakikana kuunda maneno kutokana na yale waliyopewa. Katika uundaji huu, sheria fulani lazima zizingatiwe. Mwishowe majibu kwa swali hilo yanatolewa na huwa yamepinduliwa ili kumfanya mtoto asiyasome kabla ya kumaliza zoezi hilo. Hii ina maana kuwa mtoto anayeamua kufanya zoezi hili anatakiwa kuwa mwaminifu kwake mwenyewe kwa kutoangalia majibu kabla hajamaliza kuandika. Na vile vile anaweza kuchukuwa fursa hii akajipima uwezo wake wa kujenga misamiati. Kwa mfano, katika gazeti la Alhamisi 9, 2014, Uk.8, watoto walihitajika kufauta maagizo haya:

Word Maker

By *Felix K. Magezi*

*How many words can you make from the letters in the box below? The rules are simple*

- *Each word must start with the highlighted letter.*
- *Each letter must appear only once*
- *No plurals*
- *No verbs ending in 's'.*
- *No words with hyphens or apostrophes*

| | | |
|---|---|---|
| A | o | R |
| S | I | G |
| E | T | L |

Solution: Score:15 or more- very good

**Majibu**

*Sail, sailor, soil, soar, solar, sola, stage, sit, silt, star, stare, sore, sale, site, sitar, sage, store, stir, set, sot, slot, seal, sea sore, sole, sera.*

Kwa mujibu wa Guenther na Bushman (1984), mazoezi ya aina hii huchangia kwa mbinu ya mafundisho ya mwanafunzi kutenda huku akijifunza.

Vile vile katika sehemu hii ya gazeti kuna maswali ya aina mbalimbali yanayohusu kupima masuala ya historia, jiografia, dini na siasa na fasihi simulizi hasa vitendawili. Maswali haya yanalenga kumfikirisha mtoto na hivyo basi kutimiza lengo mojawapo la magazeti na fasihi kwa kitengo hiki cha wanajamii.

Gazeti la *Sunday Nation* hutenga takribani kurasa tano au sita kwa kuwa hushughulikia mambo mengi. Kwa mfano, namna watoto husherekea siku ya kuzaliwa kwao pamoja na picha za wale wanaosherehekea siku hiyo, barua inayoandikwa na mtoto kuhusu hali fulani wanazopitia, nukuu za watu mashuhuri kutoka nchi mbalimbali, maswali kwa watoto kuhusu burudani zao, utafutaji wa marafiki-*penpal,* futuhi ya *Linda* na *Sara na Mambo.* Linda ni mhusika katika futuhi hii na kila mara yeye hutenda mambo ya kuchekesha. Watoto wanaweza kujitambulisha na mhusika huyu..

Vile vile kuna hadithi, pamoja na habari za kuwajuza watoto kuhusu vitu mbalimbali. Sehemu hii inajulikana kama, Did you Know? Swali kama hili litamfanya mtoto atake kujua ni kitu gani hicho ambacho hakijui na hivyo basi akataka kujua kwa kusoma.

Gazeti la Taifa leo huwashughulikia watoto kwa njia kama hii pia. Makala yanayowalenga husaidia kukuza mbinu zao za usomaji na hata mbinu za lugha. Kwa mfano, kuna sehemu ya Buni ambayo huwataka watoto kubuni maneno mengi iwezekanavyo ili waweze kupima viwango vyao vya kujua msamiati. Vile vile kuna sehemu ya methali, vitendawili na hata mchongoano. Watoto wenyewe hupewa nafasi ya kuunda michongoano yao.

Watoto huwa hawabanwi kwa gazeti lao ila wana uhuru wa kusoma habari mbalimbali katika gazeti kulingana na mvuto wao. Hata hivyo watoto wanahitaji kuelekezwa kwa zile mada ambazo zinawafaa.

## Namna ya kutumia magazeti darasani

Watalaamu mbalimbali wamebainisha mbinu za jinsi ya kutumia magazeti katika kuendeleza masomo (kwa mfano, Aras 2012, Babalola 2002 na wengine). Aras (keshatajwa) anadokeza kuwa picha zinaweza kuwa kichocheo cha kuwatanguliza watoto wachanga kwa fasihi.

Matumizi ya picha huwasaidia wanafunzi kupata mbinu bunifu kwa kuwamotisha na kuwafanya wawe makini kwa lile jambo wanalofanya. Vilevile picha huchangia kwa ule muktadha ambao lugha inatumika na pia huuleta ulimwengu mzima darasani, kwa mfano barabara fulani, au kitu fulani kama vile gari, treni na kadhalika.

Wanafunzi wanaweza kuelezea picha hizi kwa njia ya utonafsi (k.v. 'Hili ni gari') au au kwa njia ya kibinafsi – ('Mimi hupanda gari kila asubuhi'). Picha zaweza kutoa mwanga kwa jibu la swali fulani na zinaweza pia kutoa habari zaidi ambazo zitarejelewa katika mazungumzo, mjadala au katika hadithi.

Hivyo basi picha huweza kumfanya mwanafunzi kuwa mdadisi, kumfikirisha, kujieleza na hata kuiandikia mada fulani. Pia picha humhamasisha mwanafunzi akataka kujifunza misamiati na miundo mipya kupitia kuchochea uwezo wao wa kubuni.

Kila picha itachangia katika kumfanya mwanafunzi kusema jambo kuhusiana na picha hiyo na kisha kuandika anayofikiria. Hivyo basi, baada ya kuikagua picha fulani wanafunzi wanaweza kupewa mazoezi kama vile kuteua neno mwafuaka linaloweza kutumika kuelezaea picha hiyo.

Zaidi ya hayo, Aras (keshatajwa) anasema kuwa watoto wanaweza kupewa mazoezi ya kuandika hadithi kiwakati au wakaandika hitimisho kwa hadithi fulani wakitumia wahusika wapya na kuiweka hadithi hiyo katika mandhari mapya kimahali na kiwakati. Au wanaweza kuulizwa kuiandika hadithi hiyo upya kwa kujiweka katika nafasi ya mhusika aliye katika picha.

Wanafunzi waliokomaa kwa upande wa lugha wanaweza kuchukua nafasi ya mhusika mmoja kutoka kitabu cha fasihi, na kupitia kwa mhusika huyo wakaelekezwa kuandika barua ya kutaka ushauri nasiha kwenye gazeti. Wanafunzi wanaweza kulinganisha matukio kutoka kazi za fasihi na yale yaliyoripotiwa kwenye gazeti kisha wakahakiki matukio hayo. Vile vile wanaweza kujadili mada mbalimbali zinazoibuka katika fasihi na kwenye gazeti.

## Hitimisho

Katika kuhitimisha, ni wazi kuwa magazeti yanaweza kutumiwa kama kuchochea cha kujenga utamaduni wa usomaji miongoni mwa watoto na vijana. Muhimu ni wadau kuweka mikakati ya namna ya

kuwaelekeza wanafunzi wa viwango mbalimbali kujua namna ya kuendeleza ubunifu wao.

## Marejeleo

Aras, G. (2012). "Teaching Writing through Non- Literary Formats in the Department of English Language and Literature" katika *Frontiers of Language & Teaching*, vol. 3, pp. 132-138.

Babalola, E. (2002). Newspapers as instruments for building literate communities: The Nigerian experience. In: *Nordic Journal of African Studies*, vol.11, no. 3, pp. 403-411.

Guenther, J. Na Bushmani, J. (1984). U*sing Newspapers to Teach Secondary Language Arts*. American Newspaper Publishers Association Foundation.

Rosenblatt, L. (1995). (First published 1939). *Literature as Exploration*. New York: The Modern Language Association of America.